**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**

# MUHTASARI WA RIPOTI YA HAKI ZA BINADAMU TANZANIA 2017

Tanzania Bara

Kimetayarishwa na:

Bw. Fundikila Wazambi na Bw. Paul Mikongoti

Kimehaririwa na:

Dkt. Helen Kijo Bisimba

Bi. Felista Mauya

Wakili Anna Henga

Wakili Naemy Sillayo

Bw. Fundikila Wazambi

Bw. Paul Mikongoti

Kimechapishwa na:

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

Aprili, 2018

*Kitabu hiki hakiuzwi*

ISBN: 978-9987-740-39-0

# Yaliyomo

Kuhusu Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) .......... iii
UTANGULIZI .......... iii
SURA YA KWANZA: KUHUSU TANZANIA .......... 1
SURA YA PILI: HAKI ZA KIRAIA .......... 4
SURA YA TATU: HAKI ZA KISIASA .......... 11
SURA YA NNE: HAKI ZA KIUCHUMI .......... 13
SURA YA TANO: HAKI ZA KIJAMII NA KIUTAMADUNI .......... 15
SURA YA SITA: HAKI ZA KIUJUMLA .......... 19
SURA YA SABA: HAKI ZA MAKUNDI MAALUM .......... 20
SURA YA NANE: RUSHWA, UTAWALA BORA NA HAKI ZA BINADAMU .......... 26
SURA YA TISA: MIFUMO YA ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU .......... 28
SURA YA KUMI: MASUALA MENGINE YANAYOGUSA HAKI ZA BINADAMU .......... 30
MATATIZO YA JUMLA YANAYOATHIRI ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU .......... 31
Mapendekezo Muhimu .......... 31
Haki za Kiraia na Kisiasa .......... 31
Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni .......... 32
Haki za Makundi Maalum .......... 33

## Kuhusu Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ni shirika binafsi, huru, la hiari, lisilokuwa la kiserikali, lisofungamana na chama chochote cha kisiasa na lisilotengeneza faida kwa ajili ya kugawana, ambalo linalenga kufikia jamii yenye haki na usawa. LHRC ina lengo la kuwawezesha Watanzania ili kuendeleza, kuimarisha na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini. Lengo kubwa la LHRC ni kujenga ufahamu wa sheria na haki za binadamu miongoni mwa umma na hasa watu ambao wako kwenye hatari kubwa ya kunyimwa haki zao za msingi, kutoa elimu ya sheria na uraia, kufanya utetezi unaohusisha pia msaada wa kisheria, utafiti na ufuatiliaji wa haki za binadamu. LHRC ilianzishwa mwaka 1995 na inafanya kazi Tanzania Bara.

## UTANGULIZI

### Matukio Makubwa Yaliyoathiri au Kuimarisha Ulinzi wa Haki za Binadamu mwaka 2017

| |
|---|
| Mwanamuziki anayefahamika zaidi kwa jina la Roma Mkatoliki na wenzake waliripotiwa kutekwa na kuteswa na 'watu wasiojulikana.' |
| Ofisi za kampuni maarufu ya sheria ya IMMMA ilishambuliwa kwa kutumia bomu na 'watu wasiojulikana.' |
| 'Watu wasiojulikana' walivamia mkutano wa chama cha kisiasa cha CUF na kupiga wanachama na waandishi wa habari. |
| Kukataza mikutano ya kisiasa nje ya majimbo |
| Miili ya watu ilikutwa ndani ya viroba ikielea karibu na fukwe ya Bahari ya Hindi |
| Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) na Mnadhimu Mkuu wa Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, Tundu Lissu, alishambuliwa kwa risasi zaidi ya 30 na 'watu wasiojulikana' nje ya makazi yake Dodoma |
| Mashambulizi na mauaji ya kutisha ya askari polisi, raia na viongozi katika eneo la Kibiti na maeneo mengine ya Mkoa wa Pwani |
| Kutoweka katika mazingira ya kutatanisha kwa mwanahabari Azory Gwanda, ambaye alidaiwa kuchukuliwa na 'watu wasiojulikana' nje ya nyumba yake katika Mkoa wa Pwani |
| Matumaini ya kufutwa kwa adhabu ya kifo baada ya Rais Magufuli kukataa hadharani kusaini hati za kuwanyonga wafungwa wanaosubiri kunyongwa |
| Serikali kupambana na ukwepaji kodi kwenye sekta ya madini |
| Kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya rushwa |
| Sakata la kuondoa wafanyakazi wa umma wenye vyeti feki/vya kughushi |
| Mabadiliko makubwa katika Sheria ya Madini |
| Kuongezeka uandikishaji wanafunzi kufuatia utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo |

## Matukio ya Uvunjifu wa Haki za Binadamu

Kwa mwaka 2017, ukiukwaji wa haki za binadamu uliongezeka ukilinganisha na mwaka 2016. Haki za kiraia na kisiasa zilivunjwa zaidi, hasa haki ya kuishi, haki dhidi ya ukatili, haki ya kuwa huru na usalama wa mtu, uhuru wa kujieleza, uhuru wa kukusanyika na uhuru wa kujumuika. Kuminywa kwa haki hizi pia kuliathiri haki ya kushiriki katika utawala/serikali, hususan haki ndogo ya kushiriki katika masuala ya siasa.

*Haki 5 zilizovunjwa zaidi mwaka 2017*

| | Haki | Shida Kubwa |
|---|---|---|
| 1 | Haki ya Kuishi | Mauaji yanayotokana na kujichukulia sheria mkononi, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, mauaji ya Kibiti na maeneo mengine ya Pwani |
| 2 | Haki dhidi ya Ukatili | Ukatili wa kingono na kimwili, hasa kwa watoto (ubakaji na ulawiti) |
| 3 | Haki ya kuwa Huru na Usalama wa Mtu | Uuaji, utekaji na uteswaji unaofanywa na 'watu wasiojulikana', mauaji Kibiti na maeneo mengine ya Mkoa wa Pwani, ukamataji kinyume na sheria, kushambuliwa kwa watu, kupotea kwa mwanahabari Azory Gwanda |
| 4 | Uhuru wa Kujieleza | Kuminywa kwa uhuru wa kutoa maoni, vitisho na bugudha kwa wanahabari, matumizi ya sheria zenye vifungu tata au kandamizi |
| 5 | Uhuru wa Kukusanyika na Kujumuika | Kuminywa mikutano kisiasa, kuminywa uhuru wa kujieleza na kukusanyika, kuingilia uhuru wa asasi za kiraia wa kukusanyika |

### Madhumuni ya Ripoti na Ukusanyaji Taarifa

Lengo kubwa la ripoti hii ni kuelezea hali ya haki za binadamu kwa mwaka 2017, ikionyesha uvunjifu wa haki hizo na jitihada zilizofanywa kuzilinda. Lengo la ripoti pia ni kulinganisha hali ilivyo mwaka 2017 ukilinganisha na mwaka 2016 na pia kutumika kama nyenzo ya utetezi na kujifunzia haki za binadamu. Taarifa kwa ajili ya kuandaa ripoti hii zilikusanywa kwa njia mbalimbali, ikiwemo taarifa mbalimbali za taasisi za Serikali, Mahakama, Bunge, maafisa katika halmashauri, Jeshi la Polisi, waangalizi wa haki za binadamu, asasi nyingine za kiraia, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ya kimataifa, wateja wa msaada wa kisheria, wasaidizi wa kisheria, vyombo vya kitaifa na kimataifa vinavyosimamia haki za binadamu na vyombo vya habari.

### Muundo wa Ripoti

Ripoti ya Haki za Binadamu Tanzania 2017 imegawanyika katika sehemu 2. Sehemu ya Kwanza inaonyesha hali ya haki za binadamu kwa upande wa Tanzania Bara, huku sehemu ya pili ikionyesha hali ya haki za binadamu kwa upande wa Zanzibar. **Sura ya Kwanza** inaelezea

kuhusu Tanzania kama nchi, ikugusia kwa ufupi historia, jiografia, idadi ya watu na mihimili ya dola. **Sura za Pili hadi Sita** zinaelezea haki mbalimbali za binadamu, ambazo ni za kiraia na kisiasa; kiuchumi, kijamii na kiutamaduni; na kiujumla. **Sura ya Saba** imejikita katika haki za makundi maalum, ambayo ni wanawake, watoto, watu wenye ulemavu, wazee na watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. **Sura ya Nane** inaelezea madhara ya rushwa kwenye haki za binadamu, wakati **Sura ya Tisa** inaelezea mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu. Sura ya mwisho ni **Sura ya Kumi**, ambayo inaelezea masuala mengine ambayo yanagusa au kuathiri haki za binadamu.

# SURA YA KWANZA: KUHUSU TANZANIA

## 1.1. Historia

Kabla ya kutawaliwa na wakoloni wa Kijerumani na Kiingereza katika Karne ya 19, Tanganyika (sasa Tanzania Bara) ilikaliwa na wazawa waliokuwa wakizungumza lugha ya Kibantu, ambao baadae walipata ugeni toka Bara la Asia na toka Uarabuni. Kufikia Karne ya 15 Wareno nao wakaingia; na katika kipindi hicho cha Waarabu na Wareno, ndipo biashara ya utumwa ilipamba moto. Ilipofika mwaka 1880 ulifanyika mkutano mkubwa katika Mji wa Berlin – Ujerumani, ambapo nchi za Ulaya ziliiligawa Bara la Afrika kwa ajili ya kulitawala. Ujerumani ilipewa sehemu mbalimbali za Afrika Mashariki, ikiwemo Tanganyika. Baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, Tanganyika iliwekwa chini ya ukoloni wa Uingereza, mpaka ilipofikia mwaka 1961, ambapo Tanganyika ilipata uhuru. Katika kipindi chote cha ukoloni, machifu mbalimbali walipigana na uongozi kandamizi wa kikoloni, **ambao ulikandamiza haki zao kama binadamu**, akiwemo Mtemi Mirambo wa Wanyamwezi, Mangi Meli wa Wachagga na Abushri wa Pangani. Mapigano makubwa zaidi yalitokea Mwaka 1905 wakati wa ukoloni wa Mjerumani, yakifahamika zaidi kama *Vita vya Majimaji*, ambavyo viliongozwa na kiongozi wa kimila na kiroho aliyeitwa Kinjekitile Ngwale, ambaye aliaminika kuwa na uwezo wa kugeuza risasi kuwa maji.

Harakati za kupata uhuru ziliongozwa na chama cha TANU (Tanganyika African National Union), ambacho kilizaliwa mwaka 1954, kabla ya hapo kikifahamika kama TAA (Tanganyika African Association), kilichoanzishwa mwaka 1929. Kiongozi wa chama alikuwa Mwl. Julius Nyerere, ambaye aliiongoza TANU na Tanganyika kupata uhuru mwaka 1961, akiwa Waziri Mkuu wa Kwanza chini ya **Katiba ya Uhuru**. Mwaka 1962, Tanganyika ikawa Jamhuri, Nyerere akiwa Rais wake wa kwanza chini ya **Katiba ya Jamhuri**, ambayo ilimfanya kuwa Kiongozi wa Taifa, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu, pia akiwa sehemu ya Bunge. Mwaka 1964, Tanganyika iliungana na Zanzibar, ambayo ilikuwa imepata uhuru toka kwa Sultani wa Oman mwaka 1963, na kuunda Tanzania. Katiba ya tatu, **Katiba ya Muungano**, iliundwa, ikileta mfumo wa serikali mbili, chini ya vyama vya TANU (Tanzania Bara) na ASP (Zanzibar). Mwaka 1965, **Katiba ya Mpito** iliundwa, ambayo ilirudisha nchi katika mfumo wa chama kimoja. Katiba hii ilipitishwa kama sheria nyingine za bunge, kinyume na kanuni za kikatiba. Mwaka 1977, vyama vya siasa vya TANU na ASP viliungana na kuunda Chama cha Mapinduzi (CCM), ambacho kilitengeneza **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977**, ambayo ndio inayotumika mpaka leo, japo imekuwa ikifanyiwa marekebisho mbalimbali yapatayo kumi na nne mpaka mwaka 2015. Mojawapo ya marekebisho makubwa ni yale ya mwaka 1992, ambayo yalirudisha **mfumo wa vyama vingi**. Mengine ni yale ya mwaka 1984, ambayo hatimaye yaliingiza **hati ya haki za binadamu kwenye Katiba**. Kabla ya hapo, tangu nchi ipate uhuru, haki za binadamu hazikuonekana kuwa muhimu sana kuwekwa kwenye Katiba, japo Tanzania ilikuwa imeshaanza kuridhia baadhi ya mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu.

## 1.2. Jiografia

Tanzania iko kati ya Latitudo $1^0$ na $12^0$ Kusini na Longitudo $29^0$ na $41^0$ Mashariki. Inapakana na Bahari ya Hindi upande wa Mashariki na imepakana na nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi na Zambia kwa pande nyingine. Tanzania ndio nchi kubwa kuliko zote Afrika Mashariki na kuna Mlima Kilimanjaro, ambao ndio mlima mrefu kuliko yote barani Afrika, wa tatu duniani. Tanzania imebarikiwa kuwa na maliasili nyingi, ikiwemo mimea, mabonde ya ufa, maziwa, mito na mbuga za wanyama. Maziwa ni pamoja na Ziwa Victoria - ambalo ni kubwa kuliko yote Afrika, na Ziwa Tanganyika - ambalo lina kina kirefu kuliko yote Afrika. Mbuga za wanyama ni pamoja na Serengeti, Mikumi, Manyara, Ngorongoro na Katavi.

## 1.3. Idadi ya watu

Idadi ya watu Tanzania inaendelea kuongezeka, ambapo kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, idadi ya watu ni 43,625,354 kwa Tanzania Bara na 1,303,569 kwa Zanzibar. Wanawake ni wengi zaidi (51.3%) ukilinganisha na wanaume (48.7%). Kufikia mwaka 2016, idadi ya watu iliongezeka hadi kufikia takribani 50,144,175, huku 24,412,889 wakiwa wanaume na 25,731,286 wakiwa wanawake. Idadi kubwa ya watu wapo vijijini kuliko mijini.

## 1.4. Mihimili ya dola

Kuna mihimili mikuu mitatu ya dola nchini Tanzania, ambayo ni: Serikali, Bunge na Mahakama. Mihimili hii imeanzishwa na kupewa mamlaka na **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977**.

### A. Serikali

Serikali inajumuisha Rais - ambaye ni Kiongozi wa Taifa, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu - na Baraza la Mawaziri. Baraza la mawaziri linajumuisha Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Rais wa Zanzibar na mawaziri wote. Rais ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri. Makamu wa Rais anamsaidia Rais kwenye mambo yote ya muungano. Zanzibar ina serikali yake na Rais wake chini ya mfumo wa serikali mbili ambao Tanzania unautumia, na ina mamlaka juu mambo yote ambayo sio ya muungano, kama yalivyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

### B. Bunge

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio chombo kikuu cha kutengeneza sheria nchini, ambacho kinaundwa na wabunge mbalimbali wa chama tawala (CCM) na vyama vya upinzani. Rais pia ni sehemu ya Bunge kwa mujibu wa Katiba. Kazi kuu ya bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali. Bunge hili lina mamlaka juu ya mambo yote ya muungano. Zanzibar ina Baraza la Wawakilishi, ambacho ndio chombo chake kikuu cha kutengeneza sheria na kuisimamia

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Bunge lina wabunge wa kuchaguliwa na wabunge wa kuteuliwa.

### C. Mahakama

Mahakama ni chombo kikuu cha utoaji haki nchiniTanzania, ambapo kuna mahakama kadhaa ambazo zinatofautiana kimamlaka. Mahakama ya juu kabisa ni Mahakama ya Rufaa, ambayo ina majaji wa Mahakama ya Rufaa, ambao husimamia na kutolea maamuzi kesi zote za rufaa. Ya pili ni Mahakama Kuu, ambayo pia ina majaji (Majaji wa Mahakama Kuu), ambao husimamia kesi zote katika ngazi hiyo na kuzitolea maamuzi. Mahakama zinazofuatia ni Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo – ambayo ndio mahakama ya chini kabisa. Tofauti na mahakama za rufaa na kuu, mahakama hizi za chini zina mahakimu. Mahakama Kuu ina vitengo mbalimbali, ikiwemo cha ardhi, biashara, kazi na kingine kipya cha rushwa – ambacho kimeundwa hivi karibuni (mwaka 2016). Majaji wanateuliwa na Rais baada ya kupata ushauri wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, huku mahakimu wakichaguliwa na Tume hiyo moja kwa moja. Pia kuna **Mahakama Maalum ya Katiba**, ambayo ina mamlaka ya kushughulikia kesi za kikatiba, ikiwemo haki za binadamu. Ukiacha mahakama hizi, kuna mahakama za kijeshi-ambazo ni mahsusi kwa ajili ya wanajeshi.

Mahakama ya Rufaa ni mahakama yenye mamlaka hadi Zanzibar, ambayo pia ina mahakama zake ziitwazo Mahamaka Kuu ya Zanzibar, Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo. Pia kuna Mahakama ya Rufaa ya Kadhi na Mahakama ya Kadhi.

| Marais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
|---|
| **Mw. Julius Kambarage Nyerere: 1964-1985** |
| **Ali Hassan Mwinyi: 1985-1995** |
| **Benjamin William Mkapa: 1995-2005** |
| **Jakaya Mrisho Kikwete: 2005-2015** |
| **John Pombe Magufuli: 2015-mpaka sasa** |

# SURA YA PILI: HAKI ZA KIRAIA

**Utangulizi**

Haki Zilizoangaliwa (5)

**Haki ya Kuishi, Uhuru wa Kujieleza, Haki za Usawa mbele ya Sheria na Nafuu ya Kisheria, Haki ya Kuwa Huru na Usalama wa Mtu, Haki ya Kutoteswa**

Haki za kiraia zinalindwa kwenye mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu. Mikataba hii ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) wa mwaka 1966, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (ACHPR), Mkataba wa Nyongeza katika Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu juu ya Haki za Wanawake barani Afrika (Maputo Protocol) na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC). Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pia inajumuisha haki za binadamu, zikiwemo haki za kiraia. Ripoti hii imejikita katika haki muhimu sita, ambazo ni Haki ya Kuishi, Uhuru wa Kujieleza, Haki za Usawa mbele ya Sheria na Nafuu ya Kisheria, Haki ya Kuwa Huru na Usalama wa Mtu na Haki ya Kutoteswa. Hivyo, haki hizi zinalindwa katika ngazi za kitaifa na kimataifa na ni haki muhimu katika ufurahiaji wa haki nyingine za binadamu.


Kwa ujumla, hali ya haki za kiraia ilidorora zaidi mwaka 2017 ukilinganisha na mwaka 2016. Hii ilitokana na kuongezeka kwa vitendo vya uvunjifu au uminywaji wa haki hizo.

## 2.1. Haki ya Kuishi


Hali ya haki ya kuishi ilivunjwa zaidi kiasi mwaka 2017 ukilinganisha na mwaka 2016, sababu kubwa ikiwa ni kuendelea kwa mauaji yanayotokana na kujichukulia sheria mkononi, mauaji yanayofanywa na vyombo vya dola na mauaji yatokanayo na imani za kishirikina. Pia, haki hii ilihatarishwa na ukatili dhidi ya askari polisi. Kwa upande mwingine kulikuwa na matumaini ya kufutwa kwa adhabu ya kifo kufuatia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. John P. Magufuli, kutangaza kwamba hatosaini hati za kunyongwa kwa wafungwa waliohukumiwa kifo na kuwasamehe wafungwa 61 wa aina hiyo. Pia kulikuwa na matukio machache ya ajali za barabarani na vifo vinavyotokana na ajali hizo.

Kujichukulia Sheria Mkononi: Jumla ya matukio **479** ya kuua baada ya kujichukulia sheria mkononi yaliripotiwa polisi kati ya mwezi wa Januari hadi Juni 2017. Mpaka kufikia mwezi wa Disemba 2017, idadi ya vifo vilivyotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi ilifikia **917**, ambavyo ni **vifo 5 zaidi** ya vile vilivyoripotiwa mwaka 2016. Kwa mujibu wa takwimu za miezi 6 ya kwanza ya mwaka 2017, Mkoa wa **Dar es Salaam** unaongoza kwa matukio ya kujichukulia sheria mkononi, ukifuatiwa na **Mbeya**, **Mara**, **Geita**, **Tanga** na **Kigoma**. Kukosekana kwa imani juu ya vyombo vya usimamizi wa haki (polisi na mahakama) sababu ya rushwa iliendelea

kuwa sababu kuu ya watu kuamua kujichukulia sheria mkononi. Sababu nyingine ni pamoja na kutojua taratibu za kisheria, ikiwemo suala la dhamana.




***Mauaji yanayotokana na kujichukulia sheria mkononi 2013-2017***
*Chanzo:* Taarifa za Jeshi la Polisi





***Matukio ya Mauaji yanayotokana na kujichukulia sheria mkononi kimkoa Jan – Juni 2017***
*Chanzo:* Taarifa za Jeshi la Polisi

Mauaji yanayofanywa na Vyombo vya Dola na Ukatili dhidi ya Askari Polisi: Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kilikusanya **matukio 9 ya mauaji yanayodaiwa kufanywa na vyombo vya dola**, ambayo ni **5 zaidi ya yale yaliyokusanywa 2016**. Ripoti ya Mtazamo wa Haki za Kiraia na Kisiasa ya mwaka 2017, iliyoandaliwa na LHRC na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) inaonyesha kwamba suala la mauaji yanayofanywa na vyombo vya dola lilipata alama za chini zaidi kati ya masuala ya haki 6 yaliyofanyiwa tathmini mwaka huo. Kwa upande mwingine, kulikuwa na matukio ya kutisha ya mauaji kule Kibiti na maeneo mengine ya Mkoa wa

Pwani, ambapo **askari polisi 12 walishambuliwa na kuuwawa kikatili**, wakiwemo 8 ambao walikuwa wanarudi kutoka kufanya doria mwezi Aprili 2017.

Mauaji yanayotokana na Imani za Kishirikina na Ukatili dhidi ya Watu wenye Ulemavu wa Ngozi: **Vifo 307 vinavyotokana na imani za kishirikina** viliripotiwa mwaka 2017, ambavyo ni **47 pungufu ya vile vilivyoripotiwa mwaka 2016**. Watu 3 wa familia moja waliripotiwa kuuwawa kwa sababu hii huko Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa. Wilayani Kwimba, Mkoa wa Mwanza, mwanaume mmoja alimuua mke wake baada ya kumshutumu uchawi. Wilayani Nzega, Mkoa wa Tabora, wanawake 5 walichomwa moto hadi kufa.





*Mauaji yatokanayo na imani za kishirikina 2013 - 2017*

Sababu ya imani za kishirikina, Watu wenye Ulemavu wa Ngozi waliendelea kushambuliwa mwaka 2017 kwa ajili ya viungo vyao, japo hakuna vifo vilivyoripotiwa. LHRC ilifanikiwa kukusanya matukio 2 ya ukatili dhidi ya Watu wenye Ulemavu wa Ngozi na tukio 1 la kuharibiwa kwa kaburi la mtu aliyekuwa na ulemavu wa ngozi. Jitihada za Serikali, polisi, mahakama na asasi za kiraia zimesaidia kupunguza matukio haya, ila bado Watu wenye Ulemavu wa Ngozi wanaendelea kushambuliwa na kuishi kwa hofu. Baadhi ya wazazi na walezi mkoani Simiyu waliripotiwa **kuwapaka watoto wao wenye ulemavu wa ngozi rangi nyeusi kwenye ngozi na nywele zao ili kuwalinda na mashambulizi.**

Adhabu ya Kifo: Hakukuwa na utekelezaji wa adhabu ya kifo kwa mwaka 2017, hasa kufuatia Rais Magufuli kusema hadharani kwamba hatosaini hati za kuwanyonga wafungwa waliohukumiwa adhabu hiyo. Hii inafanya Tanzania iendelee kuonekana iko katika hali ya kuondoa adhabu ya kifo, ikizingatiwa kwamba adhabu hiyo haijatekelezwa kwa zaidi ya miaka 20 sasa. Adhabu hii ni ya kikatili na inakiuka haki ya kuishi. Hata hivyo, adhabu ya kifo inaendelea kutolewa na mahakama kwa mujibu wa sheria. LHRC ilikusanya **adhabu 15 za kifo** zalizoripotiwa na vyombo vya habari, ambazo ni **4 pungufu** ya zile zilizoripotiwa na shirika la

kimataifa la *Amnesty International* mwaka 2016. Kwa sasa, kuna **wafungwa takribani 400 waliohukumiwa adhabu ya kifo**, baada ya Rais kuwasamehe 61.

Ajali za Barabarani: Kulikuwa na ajali chache zaidi za barabarani na vifo vinavyotokana na ajali hizo (ajali 6,022 na vifo 2,705), ukilingalisha na ajali 10,292 na vifo 3,381 vilivyoripotiwa mwaka 2016. Jumla ya wanafunzi 32 wa Shule ya Msingi Lucky St. Vincent ya Arusha walikufa katika ajali mbaya iliyotokea Karatu mkoani humo.




*Ajali za barabarani na vifo 2014 – 2017*

## 2.2. Uhuru wa Kujieleza

Haki hii ilikuwa ni mojawapo ya haki zilizovunjwa zaidi mwaka 2017, kupitia kushambuliwa na vitisho kwa wanahabari, kufungiwa kwa vyombo vya habari na kutumika vibaya kwa sheria kuhusu uhuru wa kujieleza, ikiwemo Sheria ya Huduma za Habari ya 2016. Ripoti ya Mtazamo wa Haki za Kiraia na Kisiasa ya mwaka 2017 iliyoandaliwa na LHRC na ZLSC inaonyesha kwamba haki hii inaminywa zaidi kwenye kujadili masuala ya kisiasa, hivyo pia kuvunja haki ya kushiriki katika masuala ya kisiasa.

Uhuru wa Vyombo vya Habari: Matukio kadhaa ya vitisho na unyanyasaji wa wanahabari yaliripotiwa mwaka 2017, ikiwemo uvamizi wa ofisi za Clouds Media uliofanywa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na vitisho na ukamataji kinyume na sheria wa wanahabari 10 kwa amri ya mkuu mmoja wa wilaya Mkoani Arusha. Jumla ya magazeti 4 yalifungiwa na kulipishwa faini kwa sababu tofauti, ikiwemo chini ya sheria kandamizi ya Uhuru wa Vyombo vya Habari ya mwaka 2016, ambayo ina vifungu vyenye utata vinavyoweza kutumiwa vibaya. Vyombo vingine vya habari, hususani vituo vya runinga, vilipigwa faini baada ya kurusha hewani habari iliyotokana na taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu tathmini ya uchaguzi iliyotolewa na LHRC. Mwandishi wa habari kutoka Kampuni ya Mwananchi, Azory Gwanda, aliripotiwa kutekwa na watu wasiojulikana Mkoa wa Pwani mwezi Novemba 2017, na bado mpaka sasa hajapatikana wala kujulikana alipo. Mwezi wa Septemba 2017, muswada wa Kanuni za Matumizi ya Mtandao

ulitolewa, ambapo una vifungu kadhaa ambavyo vinahatarisha zaidi uhuru wa vyombo vya habari (mitandaoni) na uhuru wa kujieleza kwa ujumla. Kanuni hizi zina vifungu ambavyo vitabana uhuru wa vyombo vya habari na kutoa maoni mitandaoni. Pamoja namambo mengine, Kanuni zinapendekeza faini kubwa ya milioni 5 na kifungo cha mwaka 1 kwa kosa la kuzikiuka, malipo ya ada mbalimbali, watumiaji wa mitandao kuwajibishwa kwa taarifa zitakazoonekana ovu, zenye kutishia usalama wa nchi au za kichochezi, pamoja na watoaji huduma za mitandaoni kufunga kamera za video na kutunza kumbukumbu. Pia Kanuni zinakataza watumiaji wote wasiojulikana (anyonymous users), hali ambayo itaathiri mitandao kama *Jamii Forums*, zinaipa mamlaka Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) ya kufungia mitandao ya kijamii.

<u>Haki ya kupata Taarifa</u>: Haki ya kupata taarifa ilihatarishwa kupitia kuminywa kwa uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kutoa maoni. Kanuni za matumizi ya mtandao, kama zitapitishwa, pia zitaathiri zaidi ufurahiaji wa haki ya kupata taarifa.

<u>Uhuru wa Kutoa maoni</u>: Matukio kadhaa ya uvunjifu wa haki ya kutoa maoni yaliripotiwa mwaka 2017, ikiwemo kutishiwa na bastola kwa waziri wa zamani mwenye dhamana ya habari, Mh. Nape Nnauye, alipokuwa akijiandaa kukutana na waandishi wa habari siku moja baada ya kuondolewa kwenye nafasi ya uwaziri. Viongozi wa dini pia walikuwa na wakati mgumu kufuatia kutoa maoni yao kuhusu hali ya haki za binadamu na siasa nchini Tanzania. Mwezi Disemba 2017, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani alitishia kufuta taasisi za kidini zinazoongelea masuala ya kisiasa kwenye sehemu za ibada, akisema kwamba viongozi hao wanatakiwa kujikita kwenye masuala ya dini pekee. Mwezi huo huo, mwanafunzi mmoja wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam aliripotiwa kukamatwa na polisi baada ya kupiga picha nyufa katika hosteli mpya za chuo hicho na kuweka katika mtandao. Watu kadhaa pia walikamatwa chini ya Sheria ya Mitandaoni, ambayo ina vifungu kadhaa kandamizi. Hawa ni pamoja na Tundu Lissu kutoka CHADEMA, Zitto Kabwe kutoka ACT-Wazalendo na Sheikh Issa Ponda, ambaye ni Katibu wa Jumuiya na Taasisi za Kiislam Tanzania.

### 2.3. Haki za Usawa mbele ya Sheria na Nafuu ya Kisheria

Jitihada kadhaa zilifanywa kuongeza upatikanaji wa haki. Hata hivyo, haki za usawa mbele ya sheria na nafuu ya kisheria ziliendelea kuathiriwa na gharama za uwakilishi, upungufu wa rasilimali katika mahakama, rushwa katika mahakama na uelewa mdogo wa masuala ya kisheria.

<u>Upatikanaji wa Haki</u>: Upatikanaji wa haki uliendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizi ni pamoja na upungufu wa mawakili – ambao unaathiri haki ya uwakilishi, ucheleweshaji katika uchunguzi unaofanywa na maafisa wa dola, rushwa, kutojua sheria na taratibu za kisheria, upungufu na umbali wa mahakama, upatikanaji kidogo wa msaada wa kisheria na gharama za kupata ushauri wa kisheria na uwakilishi – suala ambalo ni mojawapo ya vikwazo katika kufikia haki, kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa. Kwa sasa kuna **Wakili mmoja (1) kwa kila watu 7800** nchini Tanzania, ambayo bado ni idadi ndogo. Wakati wa uapishwaji

wake mwezi Septemba 2017, Jaji Mkuu wa Tanzania, Mh. Prof. Ibrahim Hamis Juma, alisema kwamba **wakati Tanzania ina kata zaidi ya 3000, ni kata 976 tu ndio zina mahakama za mwanzo. Kimahitaji, kila kata inatakiwa iwe na angalau mahakama ya mwanzo moja (1).** Rushwa katika mahakama imesambaa zaidi katika mahakama za chini (Mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Hakimu Mkazi), ambazo ndio kimbilio kubwa kwa Mtanzania wa kawaida.

Katika kupunguza changamoto za upungufu wa mahakama kama ilivyoelezewa hapo juu, mpaka kufikia mwezi Juni 2017, mhimili wa Mahakama ulikuwa umejenga mahakama moja ya mwanzo na mahakama moja ya wilaya katika Wilaya ya Kibaha, Mkoa wa Pwani, kwa mujibu wa Waziri wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi kwenye hotuba yake ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 . Waziri Kabudi aliongeza kwamba mhimili wa Mahakama uliendelea na ujenzi wa mahakama za wilaya maeneo ya Bagamoyo, Mkuranga, Kigamboni na Kinyerezi-Dar es Salaam, pamoja na mahakama ya mwanzo Kawe-Dar es Salaam. Maeneo mengine ambayo alisema ujenzi ulikuwa ukiendelea mwaka 2017 (mahakama za mwanzo) ni pamoja na Mkalama, Ngorongoro, Korogwe, Kondoa, Karatu, Mvomero na Kilwa. Kwa mujibu wa mhimili wa Mahakama, jengo moja (1) la Mahakama ya Rufaa, majengo 30 ya Mahakama Kuu, majengo 24 ya mahakama za hakimu mkazi, majengo 109 ya mahakama za wilaya na majengo 150 ya mahakama za mwanzo yatajengwa kufikia mwaka 2020, kupitia mpango wa miaka 5 wa uendelezaji wa miundombinu ya mahakama (2015/2016-2019/2020). Kama haya yatafanyika kufikia mwaka 2020 kama ilivyopangwa, yatasaidia kuboresha kwa kiasi kikubwa ufikiaji wa mahakama na haki. LHRC itafuatilia ujenzi wa majengo haya ya mahakama na kuelezea hatua zilizofikiwa kupitia ripoti zake za haki za binadamu za mwaka 2018, 2019 na 2020. Katika hatua nyingine ya kuboresha upatikanaji haki, Bunge lilitunga **Sheria ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017**, ambayo inawatambua wasaidizi wa kisheria kama watoaji rasmi wa msaada wa kisheria.

<u>Haki ya Uwakilishi wa Kisheria</u>: Japokuwa LHRC haikupokea malalamiko kuhusu kunyimwa haki ya uwakilishi, ilibaini kwamba bado ubora wa uwakilishi ni changamoto kwa wananchi wengi, ambao ni maskini na hivyo hawawezi kuwalipa mawakili wabobevu. Rushwa inaathiri pia haki hii kwa kiasi kikubwa.

<u>Haki za Kusikilizwa kwa Haki na Nafuu ya Kisheria</u>: Changamoto za upatikanaji wa haki, ikiwemo upungufu wa maafisa wa mahakama, ucheleweshaji katika kesi na rushwa ni baadhi ya mambo yaliyoendelea kuathiri haki hizi nchini Tanzania mwaka 2017. Haki ya kusikilizwa kwa haki imeendelea kuwa changamoto kubwa kwa wananchi maskini, ambao hawana fedha za kuwalipa mawakili wazuri.

### 2.4. Haki ya Kuwa Huru na Usalama wa Mtu

Haki ya kuwa huru na usalama wa mtu ilihatarishwa kupitia matukio kadhaa ya ukamataji na uwekaji kuzuizini kinyume na sheria, kutekwa, kutoweka na mauaji.

Uhuru wa Kutokamatwa na Kuwekwa Kizuizini kinyume na sheria: LHRC ilikusanya matukio zaidi ya 15 ya ukamataji na uwekaji kizuizini kinyume na sharia, ikiwemo ukamataji kinyume na sheria wa walinzi wa haki za binadamu waliohudhuria uzinduzi wa kitabu jijini Dar es Salaam; ukamataji kinyume na sheria kwa amri za Wakuu wa Mikoa na Wilaya; ukamataji kinyume na sheria wa Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS); na ukamataji na uwekaji kizuizini kinyume na sheria wa viongozi na wanachama wa vyama vya siasa vya upinzani.

Haki ya Usalama wa Mtu: LHRC ilikusanya matukio takribani 38 ya uvunjifu wa haki ya usalama wa mtu, ikiwemo watu kutekwa au kupotea katika mazingira ya kutatanisha; miili ya watu ambao inaonekana waliuwawa na kuwekwa kwenye mifuko ya sandarusi ikielea kwenye fukwe za Bahari ya Hindi; mauaji ya mwanaharakati wa wanyamapori; shambulio la Rais wa Chama cha Wanasheria Tangayika (TLS), Mbunge wa Singida Mashariki na Mnadhimu Mkuu Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, Tundu Lissu; na mauaji ya raia, viongozi na askari/maafisa wa polisi kule Kibiti na maeneo mengine ya Mkoa wa Pwani, ambapo watu wasiopungua 40, wakiwemo askari/maafisa wa polisi 12, wameuwawa tangu mwaka 2015.

Haki ya Kupata Dhamana: Katika hukumu yake ya mwaka 2017 kuhusu kesi ya kupinga kifungu cha 148(4) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Mahakama Kuu iliimarisha ulinzi wa haki ya kupata dhamana. Mwaka 2015, Wakili Jeremiah Mtobesya alifungua kesi katika Mahakama Kuu kupinga mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuzuia dhamana chini ya kifungu hicho, akiomba Mahakama itamke wazi kwamba kinakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Katika hukumu yake, Mahakama Kuu ilikubaliana na Wakili Mtobesya kwamba kifungu hicho kinakiuka Katiba kwa kuvunja haki ya mshitakiwa kusikilizwa na kukata rufaa dhidi ya maamuzi ya Mkurugenzi wa Mashtka chini ya Ibara ya 13(6(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano waTanzania.

## 2.5. Haki ya Kutoteswa

Kwa mwaka 2017, LHRC ilikusanya matukio yasiyopungua 22 ya uteswaji, mengi (15) yakiwa ni ya hukumu ya kifo – ambayo ni uteswaji kwa mujibu wa Mkataba dhidi ya Uteswaji na pia inakiuma haki ya kuishi. Matukio hayo ni pamoja na kutekwa na kuteswa kwa msanii Roma Mkatoliki na wenzake. Pia, matukio kadhaa ya watoto kuteswa kama sehemu ya ukatili dhidi ya watoto yaliripotiwa. Hata hivyo, ni matukio machache ya kuteswa ambayo huwa yanakusanywa, yakiwemo ya uteswaji wa watuhumiwa unaofanywa na polisi. Changamoto nyingine katika kupambana na uteswaji ni Tanzania kutoridhia Mkataba dhidi ya Mateso na Adhabu au Vitendo vingine vya Kikatili, visivyo vya Kibinadamu, vya Kinyama na vyenye Kudhalilisha wa Mwaka 1984, ambao unajulikana pia kama Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Uteswaji.

# SURA YA TATU: HAKI ZA KISIASA

**Utangulizi**

| Haki Zilizoangaliwa (3) |
| --- |
| **Uhuru wa kukusanyika, Uhuru wa Kujumuika, Haki ya Kushiriki katika Utawala au Serikali** |

Kama ilivyo kwa haki za kiraia, haki za kisiasa zinalindwa kwenye mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu. Mikataba hii ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) wa mwaka 1966, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (ACHPR), Mkataba wa Nyongeza katika Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu juu ya Haki za Wanawake barani Afrika (Maputo Protocol) na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC). Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pia inajumuisha haki za binadamu, zikiwemo haki za kisiasa.

## 3.1. Uhuru wa Kukusanyika

Haki ya uhuru wa kukusanyika iliendelea kuwa changamoto na kuvunjwa zaidi mwaka 2017, hasa kufuatia kuzuia mikutano ya hadhara ya kisiasa, isipokuwa ndani ya jimbo la kiongozi husika wa kisiasa ambaye amechaguliwa kama mwakilishi katika jimbo au sehemu husika ndani ya jimbo. Pamoja na kwamba hakuna sheria inayosema ni lazima kufanyia mikutano ndani ya jimbo la kiongozi wa kisiasa pekee, viongozi kadhaa wa vyama vya upinzani walikamatwa kwa kwenda kinyume na amri ya kutofanya mikutano nje ya majimbo yao. Kwa mfano, zaidi ya viongozi na wanachama 53 wa vyama hivyo, wengi wao toka CHADEMA, waliripotiwa kukamatwa kwa kufanya mikusanyiko isivyo halali. Jeshi la polisi pia lilifuatilia kwa karibu hata mikutano ya asasi za kiraia (ambayo hufanyikia ndani) likihofia kwamba 'inaweza kuwa ni ya kisiasa au yenye msukumo wa kisiasa,' Mwezi Juni 2017, polisi walizuia mkutano wa uzinduzi wa kitabu kilichoandikwa na mwanaharakati wa haki za binadamu kuhusu harakati za haki za binadamu vyuoni, ambapo walimkamata, kumfungulia mashtaka na baadaye kumwachia kwa dhamana, Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Bw. Onesmo Olengurumwa.

## 3.2. Uhuru wa Kujumuika

Uhuru wa kujumuika uliathiriwa kwa kiasi kikubwa na uminywaji kinyume na sheria wa uhuru wa kukusanyika. Haki hizi mbili huwa zinaendana, na ndio maana hata katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 zimewekwa pamoja (Ibara ya 20). Kama ambavyo **Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu** iliamua katika kesi ya mtandao wa kimataifa wa kupinga uteswaji dhidi ya nchi ya Zaire (***the World Organization against Torture et al v. Zaire***) ya mwaka1996, **kutoruhusu vyama vya upinzani kufanya mikutano ya hadhara na ndani na kuwabughudhi au kuwanyanyasa kunavunja haki yao ya uhuru**

**wa kujumuika**. Mwezi Februari 2017, Waziri wa zamani wa Katiba na Sheria, Mh. Harrison Mwakyembe, alitishia kukifuta Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kwa kile alichokiita 'dalili za TLS kujiingiza katika siasa.'

### 3.3. Haki ya Kushiriki katika Utawala au Serikali

Haki ya kushiriki katika utawala au kushiriki katika serikali inajumuisha haki ya kupiga na kupigiwa kura na haki ya kushiriki katika masuala ya siasa.

<u>Haki ya Kupiga na Kupigiwa Kura</u>: Mwezi Novemba 2017, Watanzania katika kata 43 za mikoa 19 ya Tanzania Bara walifurahia haki yao ya kupiga kura wakati wa uchaguzi wa madiwani. LHRC ilifuatilia kwa karibu kampeni na uchaguzi na kuibua matukio mbalimbali ambayo yaliharibu uchaguzi na kupelekea uvunjifu wa haki za binadamu, ikiwemo matumizi ya nguvu kupita kiasi yaliyofanywa na polisi; utekaji wa viongozi wa kisiasa, wawakilishi na wapiga kura wa maeneo husika; na kupigwa na kuteswa.

<u>Haki ya Kushiriki katika Masuala ya Siasa</u>: Haki ya kushiriki katika masuala ya siasa ilivunjwa kwa kiasi kikubwa mwaka 2017, ikichangiwa zaidi na **uminywaji kinyume na sheria wa haki za ushiriki**, ambazo ni: **uhuru wa kujieleza**, **uhuru wa kukusanyika** na **uhuru wa kujumuika**. Haki ya elimu ni haki nyingine muhimu ya ushiriki, lakini kama inaovyoelezewa katika Sura ya Tano ya Ripoti, haki hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinaathiri ubora wa elimu. Tofauti na ambavyo baadhi ya maafisa au viongozi wa serikali walionekana kufikiri mwaka 2017, **haki hii ni ya kila mtu/Mtanzania**, wakiwemo viongozi wa dini; na hivyo hakuna haja ya kuwashutumu au kuwatishia viongozi wa dini pale ambapo 'wanatoa maoni kuhusu masuala la kisiasa.' Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na mikataba mbalimbali ya haki za binadamu ambayo Tanzania imeridhia, haki za kisiasa, **ikiwemo kushiriki katika masuala ya siasa,** ni za watu wote. Hivyo basi, siasa sio za wanasiasa peke yao, bali Watanzania wote!

# SURA YA NNE: HAKI ZA KIUCHUMI

**Utangulizi**

Haki Zilizoangaliwa (2)

**Haki ya Kumiliki Mali, Haki ya Kufanya Kazi**

Haki hizi zinatakiwa kusimamiwa na Serikali mwaka hadi mwaka kulingana na uwepo wa rasilimali. Hata hiyo, kasi ya usimamiaji wa haki hizi imeendelea kuwa mdogo kutokana na changamoto mbalimbali.

## 4.1. Haki ya Kumilki Mali

Haki hii imejikita kwenye ardhi, ambayo kwa mujibu wa sheria za ardhi inajumuisha kila kitu kilichojengwa juu yake. Kulikuwa na matukio kadhaa ya uvunjifu wa haki ya kumiliki mali ambayo yaliripotiwa mwaka 2017, ikiwa ni pamoja na ubomoaji wa nyumba zilizodaiwa kuwa katika hifadhi ya Barabara ya Morogoro jiijini Dar es Salaam. Baadhi ya wamiliki wa nyumba zilizobomolewa walidai kuwa na nyaraka halali za umiliki wa nyumba hizo na walikwenda mahakamani kuomba zuio la ubomoaji kwa muda. Migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali ya Tanzania pia iliendelea kuathiri ufurahiaji wa haki ya kumiliki mali. Migogoro mingi ni kati ya wakulima na wafugaji, ambayo kwa mwaka 2017 ilitokea mara kwa mara maeneo kama Kisarawe – Mkoa wa Pwani, Kilosa – Mkoa wa Morogoro na Handeni – Mkoa wa Tanga. Umiliki, upatikanaji na utumiaji wa ardhi kwa wanawake umeendelea kuwa changamoto, hasa kwa wanawake waliopo vijijini, sababu zikiwa ni pamoja na sheria baguzi za kimila na uelewa mdogo wa sheria na masuala yanayohusiana na haki ya umiliki mali. Katika zoezi la kuondoa wakulima na wafugaji katika vijiji ambavyo vilidaiwa kuwa ndani ya hifadhi na mbuga za wanyama katika maeneo mbalimbali ikiwemo ya Mkoa wa Katavi, Loliondo-Mkoa wa Arusha na Saadani-Mkoa wa Pwani, matukio mbalimbali ya uvunjifu wa haki ya kumiliki mali yaliripotiwa.

## 4.2. Haki ya Kufanya Kazi

Haki ya kufanya kazi inajumuisha <u>haki ya kupata kipato kwa kufanya kazi</u> na <u>haki ya mazingira mazuri ya kufanyia kazi</u>. Haki ya kupata kipato kwa kufanya kazi iliendelea kukabiliwa na changamoto ya ukosefu wa ajira na vijana wengi wanaomaliza elimu ya juu kukosa au kutokuwa na stadi au sifa za kuajiriwa. Kwa mujibu wa tatifi iliyofanywa na Baraza la Vyuo Vikuu la Afrika Mashariki (IUCEA) mwaka 2014, asilimia 61 ya vijana wanaomaliza elimu ya juu hawana stadi au sifa hizo, hivyo kuchangia pia ugumu wao katika kuajiriwa.

Haki ya kupata kipato kwa kufanya kazi pia iliminywa wakati wa zoezi la kuondoa wafanyakazi wenye vyeti feki/vya kughushi lililofanyika mwaka 2017. Katika zoezi hilo wafanyakazi takribani 9000 walifukuzwa kazi. Hata hivyo, kati yao 1500 walikata rufaa dhidi ya kuondolewa kwao kazini, ambapo 450 waliripotiwa kurudishwa kazini baada ya kuonekana walifukuzwa au

kuachishwa kazi kimakosa. LHRC inatoa wito kwa Serikali kufanya mazoezi kama haya kwa umakini zaidi ili kutoathiri haki za watu wambao hawana makosa.

Haki ya mazingira mazuri ya kufanyia kazi iliathiriwa pia na changamoto mbalimbali kama mshahara/ujira mdogo, ikiwemo kwa Watanzania wanaofanya kazi katika viwanda vinavyomilikiwa na wageni; mazingira mabaya ya kufanyia kazi katika sekta muhimu kama elimu, mahakama na afya, ikiwemo upungufu wa vifaa na majengo; upungufu wa rasimali watu kwenye sekta muhimu kama afya na elimu hivyo kupelekea wafanyakazi waliopo kufanya kazi kupita kiasi na kupunguza ufanisi, na muda mwingi kutolipwa kwa kufanya kazi zaidi ya muda wa kazi; na utekelezaji na usimamizi usioridhisha wa sheria za kazi, hasa katika sekta isiyo rasmi. **LHRC pia imeona kwamba muingiliano wa kisiasa katika kazi za kitaalamu unazuia wataalamu kufanya kazi kwa uhuru**. Kupitia msaada wa kisheria ambao LHRC hutoa, imebainika pia kwamba malalamiko/kesi za wafanyakazi wa kada mbalimbali kurubiniwa na kudhulumiwa sababu ya uelewa wao mdogo wa haki za mfanyakazi ni nyingi.

# SURA YA TANO: HAKI ZA KIJAMII NA KIUTAMADUNI

**Utangulizi**

| Haki Zilizoangaliwa (5) |
| --- |
| **Haki ya Elimu, Haki ya Afya, Haki ya Kupata Maji Safi na Salama, Haki ya Kuishi katika Hali Inayofaa, Haki ya Utamaduni** |

Haki za kijamii ni pamoja na Haki ya Elimu, Haki ya Afya, Haki ya kupata Maji Safi na Salama, Haki ya Kuishi katika Hali Inayofaa na Haki ya Utamaduni. Haki hizi zinalindwa katika Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni wa mwaka 1966 na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu wa mwaka 1981, ambayo Tanzania imeridhiria. Haki hizi pia zinapatikana katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Kama ilivyo kwa haki za kiuchumi, Serikali ina jukumu la kuhakikisha haki hizi zinafurahiwa na Watanzania kulingana na upatikanaji wa rasilimali. Serikali ina jukumu kubwa la kutengeneza mazingira wezeshi kuhakikisha kuwa haki hizi zinafurahiwa.

## 5.1. Haki ya Elimu

Serikali kuleta sera ya elimu bila malipo kumesaidia kuimarisha upatikanaji wa elimu ya awali na elimu msingi - ambayo sasa inaenda mpaka Kidato cha Nne, badala ya Darasa la Saba kama ilivyokuwa huko nyuma. Hata hivyo, mwaka 2017 haukuwa mzuri wa wasichana wanaopata mimba wakiwa shuleni baada ya Serikali kutoa tamko kwamba kuanzia sasa wanafunzi wanaopata mimba wakiwa shuleni hawataruhusiwa kurudi shule (za Serikali) kuendelea na masomo. Katazo hili inawezekana likawa limetolewa kwa nia njema ya kukomesha mimba za utotoni, hata hivyo linakiuka haki ya msingi ya mtoto wa kike kupata elimu ambayo inalindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia, ikiwemo Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa mwaka 1990 na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto wa mwaka 1989. Ni kwa sababu hii, mwezi Juni 2017, watetezi wa haki za binadamu na wadau wengine wa haki ya elimu walitoa tamko la kupinga uamuzi huu wa Serikali na kumwomba Rais abadilishe msimamo wake kwenye suala hili. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora pia ilitoa tamko na kuelezea kwamba hakuna sheria inayomzuia mtoto wa kike kurudi shuleni baada ya kujifungua. Hata hivyo, Serikali bado imeendelea kushikilia msimamo wake.

> Elimu msingi sasa ni miaka 10 (miaka 6 elimu ya msingi na miaka 4 elimu ya sekondari mpaka Kidato cha Nne).

Kumkatalia mtoto wa kike kurudi shule sio suluhisho la mimba za utotoni.
Kumkatalia mtoto wa kike kurudi shule kunarudisha mzigo kwa Serikali na kwenye jamii kwa ujumla.
Kumkatalia mtoto wa kike kupata elimu sababu ya kupata mimba ni ubaguzi, ambao umekatazwa katika Katiba na mikataba mbalimbali ambayo Tanzania imeridhia, ikiwemo Mkataba wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa mwaka 1979 na Mkataba wa Afrika wa Haki za Wanawake (Maputo Protocol) wa mwaka 2003.
Kumkatalia mtoto wa kike elimu sababu ya mimba kunamweka yeye na mtoto wake katika hatari zaidi ya umaskini na kuliongezea mzigo taifa mwisho wa siku.
Kumnyima mtoto wa kike elimu sababu ya mimba kunamweka yeye na mtoto wake katika hatari zaidi ya ukatili wa kijinsia na dhidi ya watoto.
Kumnyima mtoto wa kike elimu sababu ya mimba kunapunguza wigo wa kazi anazoweza kufanya na uwezekano wa kupata kazi nzuri na kuwa na maisha mazuri baadaye.
Kumnyima mtoto wa kike elimu sababu ya mimba kunaenda kinyume na **kanuni ya maslahi bora ya mtoto,** inayosisitizwa kwenye Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ya haki za watoto ambayo Tanzania imeridhia.

Japokuwa elimu bila malipo imeongeza upatakanaji wa elimu, kwa upande mwingine ubora wa elimu inayotolewa umekuwa changamoto zaidi kwa mwaka 2017 kutokana na mambo mbalimbali, ikiwemo fedha za ruzuku kutokidhi mahitaji pamoja na upungufu wa walimu, vyoo (na matundu ya vyoo), madarasa na nyumba za walimu. Mambo mengine ni pamoja na fedha zilizotengwa kwa ajili ya elimu kutopelekwa zote mashuleni au kwa wakati na mazingira duni ya walimu ya kufundishia. Kwa watoto wenye ulemavu, kukosekana kwa miundombinu rafiki na nyenzo za kujifunzia kunaminya zaidi haki yao ya kupata elimu bora.

**Hali ya Upungufu wa madawati, madarasa na nyumba za walimu**

| **MADAWATI** | | |
|---|---|---|
| | Sekondari | Msingi |
| Yanayohitajika | 64,675 | 397,652 |
| Yaliyopo | 36,043 | 278,443 |
| Upungufu | 28,632 | 119,209 |
| **MADARASA** | | |
| | Sekondari | Msingi |
| Yanayohitajika | 209,773 | 44,000 |
| Yaliyopo | 109,767 | 23,630 |
| Upungufu | 100,006 | 20,370 |

| NYUMBA ZA WALIMU | | |
|---|---|---|
| | Sekondari | Msingi |
| Zilizopo | 56,000 | 69,047 |
| Zinazohitajika | 11,017 | 19,500 |
| Upungufu | 44,983 | 49,547 |

*Chanzo*: Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

## 5.2. Haki ya Afya

Upatikanaji wa huduma za afya uliendelea kukabiliwa na changamoto kadhaa mwaka 2017, ikiwemo umbali mrefu kufikia huduma hizo, hasa kwa vijijini, na rushwa. Huduma bora za afya zinakabiliwa na changamoto kama upungufu wa bajeti, vitanda, rasilimali watu na madawa na vifaa tiba. Zoezi la kuondoa wafanyakazi wenye vyeti feki/vya kughushi pia liliathiri sekta ya afya, idadi ya rasilimali watu ikipungua zaidi. Vifo vya akinamama wakati wa kijifungua pia viliendelea kuwa tatizo mwaka 2017, likichangiwa kwa kiasi kikubwa na wanawake wengi kutofikia kirahisi huduma bora za afya. Kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) za mwaka 2015-16, kwa sasa vifo vya kinamama wakati wa kujifungua ni vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000, ambalo ni ongezeko kubwa ukilinganisha na vifo 454 kwa kila vizazi hai 100,000 kwa mwaka 2010.

## 5.3. Haki ya kupata Maji Safi na Salama

Tafiti za hivi karibuni zinaonyesha kwamba takribani nusu ya wananchi hawapati maji safi na salama, tatizo likiwa kubwa zaidi maeneo ya vijijini. Wanawake na watoto (hasa wasichana) wanaathirika zaidi na kutopatikana kwa maji safi na salama, wakilazimika kutembea umbali mrefu kutafuta maji. Tatizo hili pia lilionekana kuchangia ukatili wa kijinsia, hasa ukatili wa majumbani. Upungufu wa bajeti ya sekta ya maji na kucheleweshwa kwa fedha zilizotengwa kulionekana kuwa mojawajo ya changamoto zilizoathiri upatikanaji wa maji safi na salama kwa mwaka 2017.

## 5.4. Haki ya Kuishi katika Hali Inayofaa

Haki ya kuishi katika hali inayofaa inajumuisha haki ya kupata chakula na haki ya makazi yanayofaa. Haki hizi ni haki za muhimu katika kufurahia haki nyingine za binadamu.

<u>Haki ya kupata Chakula</u>: Kwa mwaka 2017, uhakika wa chakula ulihatarishwa na mambo kadhaa, ikiwemo mabadiliko ya hali hewa, bajeti finyu kwenye sekta ya kilimo na matumizi ya teknolojia na nyenzo duni za kilimo katika kuzalisha chakula. Wakulima wengi bado wanatuma nyenzo duni katika kilimo, hivyo kuzalisha mazao kidogo. Utafiti uliofanywa na asasi ya *Twaweza*, inayofanya kazi zake Afrika Mashariki, unaonyesha kwamba kulikuwa na hofu ya kupungukiwa chakula katika maeneo mbalimbali ya Tanzania, hasa maeneo ya vijijni.

Haki ya Makazi Yanayofaa: Haki hii iliathiriwa na changamoto kadhaa, ikiwemo ukuaji wa miji na makazi duni ya watu maskini wanaoishi mijini na uvunjwaji wa nyumba zilizodaiwa kuwa katika hifadhi za reli na barabara jijini Dar es Salaam. Zaidi ya nyumba 1000 zilibomolewa, hivyo kuongeza adha ya kukosekana kwa makazi yanayofaa kwa watu wa hali ya chini katika jiji hilo. Pia, kuna nyumba ambazo zilibomolewa wakati wa zoezi la kuondoa wanavijiji ambao walidaiwa kuwa ndani ya maeneo ya hifadhi na mbuga za wanyama katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara. Japokuwa inawezekana kweli wananchi waliobomolewa nyumba waliweka makazi kinyume na sheria, Serikali haiwezi kukwepa lawama katika hili ukizingatia suala la rushwa katika sekta ya ardhi, serikali za mitaa na serikali za vijiji, suala ambalo limechangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa makazi yasiyo halali kisheria, hasa ukizingatia wananchi wengine waliripotiwa pia kulipa kodi na kuwekewa huduma za maji na umeme katika makazi hayo.

## 5.5. Haki ya Utamuduni

Haki ya Utamaduni ni mojawapo ya haki za msingi za binadamu ambazo zilifurahiwa vizuri mwaka 2017, kama ambavyo ilikuwa mwaka 2016. LHRC iliona kwamba Watanzania wengi, yakiwemo makundi madogomadogo, walikuwa huru kushiriki katika masuala ya utamaduni na kutengeneza na kutumia bidhaa za kitamaduni. Serikali ilifanya kazi nzuri ya kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili, ikiongozwa na Raisi Magufuli, ambaye aliiitumia lugha hii katika vikao na mikutano tofauti, ya kitaifa na kimataifa. Pia, watu walikuwa huru kushiriki katika ibada na masuala ya utamaduni.

# SURA YA SITA: HAKI ZA KIUJUMLA

**Utangulizi**

| Haki Zilizoangaliwa (2) |
|---|
| **Haki ya Maendeleo, Haki ya Kufurahia na Kufaidika na Maliasili** |

Haki za Kiujumla ni haki ambazo zinafurahiwa na watu wengi. Haki hizi ni pamoja na Haki ya Maendeleo na Haki ya Kufurahia na Kufaidika na Maliasili.

## 6.1. Haki ya Maendeleo

Utawala wa sheria, utawala bora, ushiriki wa wananchi na uheshimu wa haki za binadamu ni mambo ya msingi katika kufurahia haki ya maendeleo. Maendeleo yanaweza kuwa ya kisiasa, kiuchumi, kijamii au kiutamaduni. Maendeleo ya kisiasa yaliingia dosari kubwa mwaka 2017 kufuatia uminywaji wa uhuru wa kujieleza na utawala wa sheria kutosimamiwa vizuri. Jitihada kadhaa zilifanywa na Serikali katika kuleta maendeleo ya kijamii katika nyanja za elimu, afya, maji na makazi. Hata hivyo, kama ambavyo imeelezewa kwenye Sura ya Tano hapo juu, upatikanaji wa huduma bora za kijamii kwa kiasi kikubwa na maeneo mengi haukuwa wa kuridhisha sababu ya changamoto mbalimbali. Kwa upande wa maendeleo ya kiuchumi, pamoja na uchumi wa Tanzania kukua katika miaka ya karibuni, kukua huko hakujaweza kwenda sambamba sana na kupunguza umaskini na tofauti kati ya walionacho na wasionacho. Bado kuna asimilia kubwa ya Watanzania wanaoishi katika lundo la umaskini (karibia asilimia 50).

## 6.2. Haki ya Kufurahia na Kufaidika na Maliasili

Jitihada za Serikali mwaka 2017 zilisaidia kukuza na kulinda haki ya kufurahia na kufaidika na maliasili, hasa mabadiliko mbalimbali katika sekta ya madini. Kwa mfano, kurekebishwa kwa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kulisaidia kufanya uwajibikaji wa makampuni kwa jamii (corporate social responsibility) kuwa ni lazima kisheria, suala ambalo linatoa fursa kwa makampuni ya madini kuwajibika zaidi kutoa huduma za kijamii katika maeneo ambayo migodi ipo. Uundwaji wa sheria mpya mbili za za maliasili pia kunaipa Tanzania uwezo wa kufanya makubaliano upya na makampuni ya madini. Hata hivyo, marekebisho haya yalifanywa haraka bila kuruhusu ushiriki zaidi wa wabunge na wadau mbalimbali. LHRC inashauri masuala ya msingi kama haya kutopelekwa haraka ili kutoa mwanya wa kujadili na kuboresha zaidi na kuzuia Serikali kuingia kwenye mitego au migogoro ya kisheria hapo baadaye.

# SURA YA SABA: HAKI ZA MAKUNDI MAALUM

**Utangulizi**

Makundi Yaliyoangaliwa (5)


**Wanawake, Watoto, Watu wenye Ulemavu, Wazee, Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI**

Haki za msingi za makundi maalum ambazo huwa zinavunjwa mara nyingi ni **Haki dhidi ya Ukatili**, **Haki ya Usawa na Kutobaguliwa**, na **Haki ya Kupata Huduma Bora za Kijamii**.

## 6.1. Haki za Wanawake

Ukiachilia mikataba mbalimbali ya haki za binadamu inayotoa ulinzi wa haki hizo kwa watu wote, kuna mikataba kadhaa ambayo ni ya haki za wanawake pekee. Mikataba hii ni pamoja na Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa mwaka 1979 na Mkataba wa Afrika wa Haki za Wanawake (Maputo Protocol). Jambo kubwa linalokatazwa katika mikataba hii ni **ubaguzi dhidi ya wanawake** unaopelekea kushindwa kufurahia haki zao muhimu kama binadamu. **Mwaka 2017, wanawake waliendelea kubaguliwa na kufanyiwa ukatili, hali iliyoathiri ufurahiaji wa haki zao za kuishi, kumiliki mali na usawa**.

<u>Ukatili dhidi ya Wanawake:</u> Mwaka 2017 wanawake walifanyiwa aina mbalimbali za ukatili ikiwemo wa kimwili na kingono. Takwimu za Jeshi la Polisi zinaonyesha kwamba jumla ya kesi za **ubakaji 2,059 ziliripotiwa kufikia mwezi Machi 2017**. Kufikia mwisho wa Disemba 2017, **matukio ubakaji yalikuwa 8,039**, **yikiongezeka kwa kiwango kikubwa** (matukio 394), ukilinganisha na matukio 7,645 ya mwaka 2016.




**Matukio ya ubakaji yaliyoripotiwa polisi 2015-2017**

Utafiti uliofanywa na LHRC katika wilaya 20 za Tanzania Bara unaonyesha kwamba aina ya ukatili dhidi ya wanawake inayofanyika zaidi ni ukatili wa kingono, hasa ubakaji, ukifuatiwa kwa karibu na ukatili wa kimwili. LHRC pia ilikusanya matukio takribani 75 ya ukatili dhidi ya wanawake kupitia vyombo vya habari, mengi yakiwa ni ya ukatili wa kimwili. Sababu za kuenea kwa ukatili dhidi ya wanawake ni pamoja na imani za kishirikina (hasa kwa wanawake wazee na wenye macho mekundu), ulevi miongoni mwa wanaume, wivu na watuhumiwa kufanya hujuma na kuwahonga wanafamilia ili kuficha ushahidi. Asilimia 16 ya matukio ya ukatili dhidi ya wanawake yaliyokusanywa na LHRC yalisababishwa na wivu.


Usawa wa Kijinsia na Kutobaguliwa: Lengo la 5 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) linasisitiza usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake na wasichana wote. Jitihada kadhaa zimeendelea kufanywa kuelekea kufikia lengo hili, ikiwemo kupitishwa kwa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutokomeza Aina zote za Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18-2021/2022). Hata hivyo, bado kuna changamoto kadhaa katika kufikia lengo hili (kufikia 50-50), ikiwemo kupungua kwa uwakilishi wa wanawake katika nafasi za maamuzi katika Serikali ya Awamu ya Tano ukilinganisha na Serikali ya Awamu ya Nne, ukiacha majaji na wabunge wanawake - ambao idadi yao iliongezeka kidogo katika Serikali ya Awamu ya Tano. Mfano mzuri ni kwa **wakuu wa mikoa, mawaziri na manaibu waziri, ambapo inaonekana kwamba kuna wakuu wa mikoa 5 wanawake katika mikoa 31 ya Tanzania Bara, mawaziri 4 tu na manaibu waziri 8 kati ya 19**. Pia, kuna changamoto ya kunyimwa au kutopewa fursa ya kumiliki mali na kupata urithi. Wajane pia wameendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali katika kufurahia haki zao, hasa haki ya urithi, sababu ya sheria za kimila ambazo zinabagua wanawake katika umiliki wa mali.

### 6.2. Haki za Watoto

Haki za watoto zinalindwa katika mikataba mikubwa miwili ya haki za watoto, ambayo ni: Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (CRC) wa mwaka 1989 na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) wa mwaka 1990, yote ikiwa imeridhiwa na Tanzania. Kwa hapa nchini Tanzania pia tuna Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ambayo inataja haki za msingi za mtoto kama zilivyoelezewa kwenye mikataba hiyo na kueleza wazi kwamba katika kufanya maaumuzi yoyote kuhusu mtoto **kanuni ya maslahi bora ya mtoto** lazima izingatiwe. Mikataba hii na sheria ya mtoto inatoa wajibu kwa Serikali, wazazi, walezi na wanajamii kwa ujumla kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vyote vya ukatili na ubaguzi. Hata hivyo, watoto wameendelea kuwa wahanga wa aina mbalimbali za ukatili, hasa ukatili wa kingono (ubakaji na ulawiti).

Ukatili wa Kingono: Takwimu za Jeshi la Polisi za mwaka 2017 zinaonyesha picha mbaya zaidi ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto, ambapo **jumla ya matukio 13,457 ya ukatili dhidi ya watoto** yaliripotiwa, **mengi yakiwa ni ya ubakaji na ulawiti**. Matukio haya ni mengi sana ukilinganisha na matukio 10,551 yaliyoripotiwa mwaka 2016.

Utafiti uliofanywa na LHRC kupitia vyombo vya habari (magazeti na televisheni) ulionyesha kwamba **asilimia 85 ya matukio ya ukatili dhidi ya watoto yalikuwa ni ya ukatili wa kingono**, hasa ubakaji na ulawiti. **Wahanga wengi walikuwa ni watoto wa shule za msingi wenye miaka kati ya miaka 7 hadi 14**. **Cha kusikitisha zaidi, mmojawapo wa wahanga alikuwa ni mtoto wa miaka 2!** Pia, LHRC ilikusanya **matukio 3 ya watoto ambao walibakwa na baba zao!** Matukio 7 kati ya matukio ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto yaliyokusanywa na LHRC yalihusu **ubakaji na ulawiti wa watoto wenye umri mwaka 1 hadi 6!**





**Asimilia ya matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliyokusanywa na LHRC Mwaka 2017**

Matukio ya ukatili dhidi ya watoto huwaathiri sana watoto kisaikolojia kwa maisha yao yote na pia hupelekea hata kifo. Mfano, mtoto mmoja aliripotiwa kubakwa hadi kufa mkoani Katavi mwezi Juni mwaka 2017. Tukio kama hilo pia liliripotiwa mkoani Mwanza.

<u>Ukatili wa Kimwili na Kisaikolojia</u>: Matukio kadhaa ya ukatili wa kimwili na kisaikolojia dhidi ya watoto yaliripotiwa mwaka 2017. Baadhi ya matukio hayo yalikuwa mabaya sana kiasi cha kusababisha vifo vya watoto. Mojawapo ya matukio hayo lilitokea Mbulu-Mkoa wa Manyara, ambapo baba alimpiga hadi kumuua mwanawe wa miaka 6 baada ya kupoteza mbuzi 5. Tukio jingine lilitokea Sumbawanga-Rukwa, ambapo baba mmoja alikamatwa kwa kumuua mtoto wake wa miaka 2, akisema alifanya hivyo kwa sababu alikuwa hampendi! Matukio mengi yaliyoripotiwa ya aina hii ya ukatili yalitokea nyumbani.

<u>Mila zinazoathiri haki za Mtoto</u>: Mila hizi ni pamojana ndoa za utotoni na ukeketaji.
Ndoa za Ututoni: Chini ya Mkataba wa Haki za Wanawake wa Afrika (Maputo Protocol), Tanzania ina wajibu wa kuchukua hatua mbalimbai za kisheria kuhakikisha umri wa chini wa kuolewa ni miaka 18. Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) unakataza ndoa za utotoni. Hata hivyo, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 bado inaruhusu wasichana wenye umri wa miaka 14 na 15 kuolewa. Mwaka 2016, Mahakama Kuu ya Tanzania ilitoa hukumu katika *Kesi ya Rebecca Gyumi* iliyofunguliwa na asasi inayojishughuisha na haki za mtoto wa kike ya

*Msichana Initative*, ambapo ilitamka kwamba vifungu kwenye Sheria ya Ndoa vinavyoruhusu wasichana wenye miaka 14 na 15 kuolewa vinakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kuitaka Serikali irekebishe sheria hiyo. Hata hivyo Serikali imeamua kukata rufaa na kwa sasa kesi ipo kwenye Mahakama ya Rufaa. Wakati huo, watoto wa kike bado wanaendelea kuwa katika hatari ya kuolewa, hivyo kuwanyima haki za za msingi, ikiwemo elimu na usawa, huku ikiwaweka katika hatari zaidi ya kufanyiwa ukatili wa kijinsia. Mkoa wa Shinyanga (59%) ndio unaoongoza kwa ndoa za utotoni, ukifuatiwa na Tabora (58%) na Mara (55%).




**Asilimia za ndoa za utotoni kimkoa**

Ukeketaji: Juhudi zinazofanywa na wadau mbalimbali, ikiwemo Serikali, polisi na asasi za kiraia zimesaidia kupunguza matukio ya ukeketaji, ambao ni kosa la jinai (ukifanywa kwa watoto) ambapo kwa sasa ukeketaji umepungua kutoka asilimia 15 mwaka 2010 hadi asilimia 10 mwaka 2016, kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Hata hivyo, matukio kadhaa ya ukeketaji yaliripotiwa, ikiwemo tukio moja mkoani Manyara ambapo msichana mmoja alinusurika kufa baada kutokwa na damu nyingi baada ya kukeketwa. Mkoani Arusha polisi waliripoti kuwatafuta wazazi wa **msichana mmoja ambaye alitokwa damu hadi kufa baada ya kukeketwa**. Tafiti pia zinaonyesha kubadilishwa kwa mbinu za ukeketaji, ikiwemo kuwakeketa watoto wachanga mara baada ya kuzaliwa.

**Mikoa inayoongoza kwa ukeketaji ni Manyara (58%), Dodoma (47%), Arusha (41%), Mara (32%), na Singida (31%).**

## 6.3. Haki za Watu wenye Ulemavu

Kuna mkataba maalum wa kimataifa unaolinda haki za watu wenye ulemavu, uitwao Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu (CRPD). Haki hizo ni pamoja na haki ya usawa na kutobaguliwa, haki ya kuishi, haki ya usawa mbele ya sheria, haki ya kuwa huru na usalama wa mtu, haki ya kutoteswa, haki dhidi ya ukatili, haki ya elimu, haki ya afya na haki ya kufanya kazi na kuajiriwa. Mkataba huu umeridhiwa na Tanzania na kutungiwa Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2010. Watu wenye ulemavu wanahitaji huduma maalum zitakazowawezesha kufurahia haki za binadamu sawa na watu wengine.

Kwa mwaka 2017, watu wenye ulemavu waliendelea kukumbwa na changamoto mbalimbali ambazo ziliwafanya wasifurahie vizuri haki zao kama binadamu. Changamoto kubwa ni ubaguzi, ikiwemo katika kupata huduma za afya, elimu na miundombinu. Watu wenye ulemavu pia walikumbwa na changamoto ya kufanyiwa aina mbalimbali za ukatili, hasa wa kimwili na kisaikolojia, iwemo kuitwa majina mabaya. Kwa upande wa watu wenye ulemavu wa ngozi, waliendelea kuishi kwa hofu ya kuuwawa au kushambuliwa kwa ajili ya viungo vyao kutokana na imani za kishirikina, kama ilivyoelezwa katika Sura ya Pili ya Ripoti. Mwezi Juni 2017, video za watu wenye ulemavu waliokuwa wakiandamana jijini Dar es Salaam wakiburuzwa na kupigwa na polisi zilisambaa mitandaoni, mfano mwingine wa matumizi ya nguvu kupita kiasi. Kitendo hichi kilikemewa vikali na wadau wa haki za binadamu, ikiwemo LHRC na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Waziri wa Mambo ya Ndani, Mh. Mwigulu Nchemba alikiri kwamba polisi walitumia nguvu kupita kiasi na kuomba radhi kwa niaba. Hata hivyo, hakukuwa na taarifa ya hatua zozote za kinidhamu zilizochukuliwa dhidi ya askari polisi waliohusika.

### 6.4. Haki za Wazee

Tofauti na makundi mengine, hakuna mkataba maalum wa kulinda na kusimamia haki za wazee. Hata hivyo, kama binadamu wengine, wazee wana haki mbambali za binadamu kama zilivyoanishwa katika mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa, ikiwemo Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (ACHPR). Wazee walikumbwa na changamoto mbalimbali mwaka 2017 ambazo ziliwazuia kufurahia kikamilifu haki zao kama binadamu, changamoto kubwa ikiwa ukatili dhidi yao. Kama ilivyoelezwa katika Sura ya Pili ya Ripoti, wazee (hasa wanawake) ndio wahanga wakubwa wa mauaji yanayotokana na imani za kishirikina. **Mkoa wa Tabora bado unaongoza kwa mauaji ya aina hii. Mikoa mingine ni pamoja na Songwe, Njombe, Mwanza, Kigoma na Shinyanga**.

Malamiko ya wazee kubaguliwa katika kupata huduma za afya (bure) pia yaliripotiwa kwa kiasi. Hata hivyo, katika kuongeza upatikanaji wa huduma hizo kwa wazee Hamalshauri ya Manispaa ya Ubungo ilitoa kadi za matibatu bure kwa wazee 7,299 mwezi Septemba 2017, huku Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ikitoa kadi kwa wazee zaidi ya 2500 mwezi Oktoba 2017.

## 6.5. Haki za Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI

> Kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), mikoa inayoongoza kwa UKIMWI ni Njombe, Iringa na Mbeya.

Watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wana haki na wajibu mbalimbali kama inavyoanishwa kwenye Sheria ya UKIMWI ya mwaka 2008, ikiwemo haki ya kutobaguliwa, haki ya kupata huduma za afya na wajibu wa kutoambukiza wengine ukimwi kwa makusudi. Sheria ya UKIMWI inakataza ubaguzi dhidi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na hili ni kosa la jinai ambalo adhabu yake ni faini isiyopungua Shilingi Milioni 2 au kifungo kisichozidi mwaka 1 au vyote. Watu hawa waliendelea kukumbwa na changamoto ya ubaguzi na unyanyapaa mitaani, kazini, kwenye vituo vya afya na shuleni, hali inayowasababisha wasifurahie kikamilifu haki zao kama binadamu. Changamoto za sekta ya afya, kama zilivyoainishwa kwenye Sura ya Tano ya Ripoti hii, zinaathiri pia upatikanaji wa huduma bora za afya kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Ukatili wa kijinsia, hasa wa kingono, pia unachangia kusambaa kwa maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

# SURA YA NANE: RUSHWA, UTAWALA BORA NA HAKI ZA BINADAMU

Rushwa huathiri uwezo wa Serikali kusimamia na kuhakikisha haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni zinafurahiwa kulingana na uwepo wa rasilimali. Matumizi mabaya ya mali za umma yanapunguza nguvu ya Serikali kuweza kutoa huduma za kijamii kama maji, elimu na afya kwa wananchi, hivyo kuathiri haki za maji, elimu na afya. Haki za kiraia na kisiasa kama vile haki ya kuishi, upatikanaji haki, haki ya usawa mbele ya sheria na haki ya kusikilizwa kwa haki pia zinaathiriwa na rushwa. Rushwa katika mfumo wa haki hutengeneza maafisa polisi, wachunguzi, mahakimu na majaji ambao ni wala rushwa na husabaisha kutokuwepo usawa mbele ya sheria na kutosikilizwa kwa haki. Rushwa wakati wa uchaguzi inaweza kuwakatisha watu tamaa kufurahia haki zao za kisiasa, kama vile haki ya kupiga kura.

Sababu kubwa ya watu kutokuwa na imani na mfumo wa haki ni rushwa, jambo ambalo husababisha waamue kujichukulia sheria mkononi. Haki ya maendeleo, ambayo ni ya mtu binafsi na kikundi cha watu, pia inathiriwa na vitendo vya rushwa. Rushwa katika kukusanya kodi maana yake ni mapato madogo kwa Serikali, jambo ambalo linaathiri upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii na miradi ya maendeleo. Utawala bora pia unaweza kuathiriwa na rushwa kwa kudhoofisha utawala wa sheria na kukandamiza demokrasia. Kwa hiyo, rushwa ni adui mkubwa wa haki za binadamu, hasa kwa nchi za ulimwengu wa tatu kama Tanzania, ambapo rushwa husababisha Serikali kupoteza hadi asilimia 20 ya bajeti yake kila mwaka, kwa mujibu wa taarifa ya shirika linalojihusisha na kukusanya taarifa kuhusu rushwa katika sehemu mbalimbali duniani lililopo nchini Norway, liitwalo *U4 Anti-Corruption Reserouce Centre*, ya mwaka 2009.

Mwaka 2017, Serikali, kupitia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ilifanya jitihada zaidi katika kupambana na rushwa. Tafiti mbili kuhusu mtazamo kuhusu hali ya rushwa nchini zilizofanywa mwaka 2017 zilionyesha kwamba rushwa inaonekana na watu wengi kupungua, huku polisi na mahakama zikiendelea kutajwa kama taasisi zinazoongoza kwa rushwa. Taarifa ya shirika la kimataifa linalojihusisha na mapambano dhidi ya rushwa la *Transparency International* kuhusu mtazamo kuhusu rushwa katika nchi mbalimbali duniani ilionyesha pia kwamba rushwa imepungua kiasi nchini Tanzania, baada ya kupata alama 36 kati ya 100, ukilinganisha na alama 32 kwa mwaka 2016. Hata hivyo, kupunguza uwazi na uminywaji wa uhuru wa kujieleza (ukijumuisha wa vyombo vya habari), ambazo ni silaha muhimu katika mapambano dhidi ya rushwa, kunaweza kurudisha nyuma juhudi hizi.

Mwaka 2017 TAKUKURU ilifanikiwa kumfungulia mashtaka Bw. James Rugemalira, ambaye alituhumiwa katika sakata la Akaunti ya Tegeta Escrow, pamoja na mwenzake Bw. Harbinder Sethi. Hata hivyo utekelezaji wa majukumu wa taasisi hii muhimu unakabiliwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo mapungufu katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka

2007 (mfano adhabu ndogo), mashtaka kufunguliwa pale ambapo tu Mkurugenzi wa Mashtaka ameridhia, upungufu wa bajeti na upungufu wa rasilimali watu.

# SURA YA TISA: MIFUMO YA ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU

**Utangulizi**

Mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu inajumuisha sheria zinazolinda haki za biandamu na taasisi mbalimbali ambazo zina jukumu la kusimamia sheria hizo na kulinda na kuimarisha haki za binadamu. Kuna mifumo ya kataifa, mifumo ya kikanda na mifumo ya kimataifa.

## 9.1. Mifumo ya Kitaifa ya Ulinzi wa Haki za Binadamu

Mifumo ya kitaifa ya ulinzi wa haki za binadamu inajumuisha taasisi muhimu kama Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), Mahakama na Vyombo vya Dola. Vyombo hivi vipo kwa mujibu wa sheria.

<u>Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora</u>: Tume hii ilianzishwa chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na jukumu lake kubwa ni kuimarisha na kulinda haki za binadamu, ikihakikisha zinaheshimiwa. Pia, Tume huishauri Serikali na taasisi zake kwenye masuala ya haki za binadamu na utawala bora na hupokea malalamiko ya uvunjifu wa haki za binadamu toka kwa wananchi na kuyafanyia kazi. Kwa mwaka 2017, Tume iliendelea na kazi zake hizi za kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu, japo bado inakabiliwa na changamoto mbambali, ikiwemo bajeti finyu, upungufu wa wafanyakazi na uchelewaji wa Serikali na watendaji wake katika kufanyia kazi mapendekezo yake.

<u>Mahakama</u>: Mahakama ni chombo muhimu sana katika ulinzi wa haki za binadamu, ambacho hutoa tafsiri mbalimbali za sheria zinazohusu haki za binadamu, husikiliza kesi na kutoa maamuzi na nafuu za kisheria. Mhimili huu ni muhimu na hutakiwa kuwa huru katika kuchunga mienendo na matendo ya mihimili mingine, ambayo ni Serikali na Bunge. Kwa mwaka 2017, Mahakama iliendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zilizoathiri ulinzi wa haki za binadamu, ikiwemo upungufu wa rasilimalli (watu na majengo) na rushwa – ambayo huchelewesha au kukosesha haki. Kama ilivyoelezewa katika Sura ya Nane ya ripoti, rushwa imetapakaa zaidi katika mahakama za chini (mahakama za mwanzo, mahakama za wilaya na mahakama za hakimu mkazi), ambazo hufikiwa na watu wengi zaidi ukilinganisha na za juu (Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa).

<u>Vyombo vya dola</u>: Hivi ni pamoja na Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza, ambavyo vina nafasi na jukumu kubwa la kulinda na kuimarisha haki za binadamu. Jeshi la Polisi lina jukumu la kusaidia watu kufikia haki kwa kufanya uchunguzi na kuwafikisha watuhumiwa au wavunjifu wa haki za binadamu mahakamani. Magereza huwalinda wanajamii dhidi ya watu waliohukumiwa kutumikia vifungo kwa kufanya uhalifu ambao unahatarisha haki za binadamu, na hivyo uwepo wake huimarisha ulinzi wa haki za binadamu. Majeshi haya, hasa Jeshi la Polisi, yalikumbwa na changamoto mbalimbali zilizoathiri ulinzi wa haki za binadamu, ambazo ni pamoja na rushwa, upungufu wa rasilimali (watu na vifaa), mazingira duni ya kufanyia kazi na magereza kujaa kupita

kiasi. LHRC imegundua kwamba bado kuna tatizo la uelewa mdogo na umuhimu wa haki za binadamu baina ya maafisa/askari polisi, hasa wa ngazi za chini. Pia, kwa upande wa kujaa kwa rumande na magereza, LHRC imeona kwamba kuongezeka kwa matukio ya ukamataji na uwekaji kuzuizini kinyume na sheria pamoja na kunyimwa dhamana kunachangia tatizo hili. LHRC imegundua pia kukosekana kwa chombo au mamlaka huru ya kuangalia na kusimamia utendaji kazi wa polisi nako kunachangia wakati mwingine kwa vyombo hivi kutumia vibaya mamlaka yake.

## 9.2. Mifumo ya Kikanda na Kimataifa ya Ulinzi wa Haki za Binadamu

Mifumo ya kikanda na kimataifa ya ulinzi wa haki za binadamu inajumuisha mikataba mbalimbali ya haki za binadamu, ambayo inaunda vyombo mbalimbali vya kusimamia utekelezaji wa mikataba hiyo na nchi wanachama. Chini ya Umoja wa Mataifa kuna mfumo wa kutathmini haki za binadamu uitwao Mpango wa Kimataifa wa Kujitathmini juu ya Masuala ya Haki za Binadamu (UPR) au Tathmini ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa, ambao unasimamiwa na Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa. Mfumo huu unalenga kuboresha hali ya haki za binadamu katika nchi 193 wanachama wa Umoja wa Mataifa. Nchi wanachama, ikiwemo Tanzania, huwasilisha ripoti kila baada ya miaka 5 ikielezea ni hatua gani imechukua kuboresha haki za binadamu kulingana na wajibu ulioanishwa katika mikataba mbalimbali ya haki za binadamu ambayo zimeridhia. Ukiacha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, vyombo vingine katika ngazi za bara na kimataifa zinazosimamia utekelezaji wa majukumu yanayohusiana na haki za binadamu katika mikataba iliyoridhiwa ni pamoja na Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa (HRC), Kamati ya Haki za Mtoto (CRC), Kamati ya Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni (CESCR), Kamati ya Kuondoa aina Zozote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW), Kamati ya Haki za Watu wenye Ulemavu (CRPD) na Kamati ya Wataalamu katika Masuala ya Haki na Ustawi wa Mtoto Afrika (ACERWC). Tanzania ina wajibu wa kutoa taarifa za haki za binadamu kwa vyombo hivi kila baada ya muda fulani. Hata hivyo, siyo mara zote ripoti hizo zimekuwa zikitumwa au kutumwa kwa wakati.

Pia, kwa upande wa Afrika kuna Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ambayo ipo Arusha – Tanzania) naTume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ambapo nchi wanachama wa Umoja wa Afrika hutakiwa kutuma ripoti na pia hupokea na kusikiliza malalamiko kuhusu haki za binadamu). Kuna taratibu za kupekeleka malalamiko ya uvunjifu wa haki za binadamu endapo mhanga wa uvunjifu huo hajaridhika na nafuu aliyopata katika mifumo ya kitaifa ya utoaji haki.

# SURA YA KUMI: MASUALA MENGINE YANAYOGUSA HAKI ZA BINADAMU

**Utangulizi**

Kwa mwaka 2017, LHRC iliona uvumilivu wa kisiasa na jukumu la wadau mbalimbali katika kuendeleza, kusimamia, kuboresha na kulinda haki za binadamu kama mambo mengine ambayo yanagusa haki za binadamu.

## 10.1. Uvumulivu wa Kisiasa

Kwa mwaka 2017, LHRC iliona kwamba kadri muda unavyokwenda ndivyo hali ya uvimulivu wa kisiasa inapungua, hasa kati ya chama tawala (CCM) na chama kikuu cha upinzani (CHADEMA). Hali hii imepelekea kuongezeka kwa chuki kati ya viongozi na wanachama ama wafuasi wa vyama hivyo na kusababisha mivutano mikubwa na uvunjifu wa haki za binadamu, ikiwemo kuminywa kwa haki za msingi kinyume na sheria. Kauli mbalimbali za kibaguzi zilizotolewa na baadhi ya viongozi, husasan wa chama tawala, zilichangia kupunguza uvumilivu wa kisiasa mwaka 2017.

## 10.2. Jukumu la Wadau Mbalimbali katika Kuendeleza, Kusimamia, Kuboresha na Kulinda Haki za Binadamu

Mwaka 2017 LHRC iliona kwamba bado kuna uelewa mdogo baina ya wadau mbalimbali kuhusu jukumu la kuboresha na kulinda haki za binadamu, wengine wakifikiria kwamba hilo ni jukumu la Serikali na baadhi ya watu katika jamii pekee (mfano asasi za kiraia). Chini ya mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu kitaifa na kimataifa, **kila mwananchi ana wajibu wa kutiii sheria na kufuata taratibu za kisheria, kutoa taarifa unapotokea uhalifu au uvunjifu wa haki za binadamu, na kuingilia kati kutetea haki ya mtu pale inapoonekana kuvunjwa**. Viongozi wa dini na wa kimila pia wana jukumu la kukemea uvunjifu wa haki za binadamu na kuasa wanajamii kuacha kuvunja haki hizo. Vyombo vya dola na habari pia vina jukumu kubwa la kulinda na kuendeleza haki za binadamu.

# MATATIZO YA JUMLA YANAYOATHIRI ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU

- Kutokuwa na Katiba madhubuti (Katiba ya Wananchi)
- Kutoheshimu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977
- Sheria mbaya, zenye mapungufu au zilizopitwa na wakati
- Uelewa mdogo wa sheria, zikiwemo zinazohusu haki za binadamu, kwa pande zote
- Kutofuata utaratibu wa kisheria
- Mapungufu ya bajeti katika sekta muhimu
- Kutotii sheria
- Uelewa mdogo wa haki za binadamu baina ya wananchi na viongozi wao
- Kukosekana uwajibakaji wa kitaasisi na hata mtu mmoja mmoja

## Mapendekezo Muhimu

### Haki za Kiraia na Kisiasa

- Wizara ya Mambo ya Ndani na Jeshi la Polisi kuhakisha kwamba pale yanapotokea mauaji yanayotokana na kujichukulia sheria mkononi na yanayofanywa na vyombo vya dola hatua zinachukuliwa haraka na wakosaji wanawajibishwa na kupelekwa mbele ya vyombo vya sheria kwa wakati;
- Serikali kutamka rasmi kwamba nchi iko kwenye hali ya kutotekeleza adhabu ya kifo na kupunguza adhabu za kifo zilizokwishatolewa kuwa za maisha jela;
- Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kupeleka muswada bungeni wa kuondoa adhabu ya kifo;
- Tume ya Haki za Binadamu na Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba maaskari na maofisa polisi wana uelewa mzuri wa Kanuni za Umoja wa Mataifa za Matumizi ya Nguvu na Silaha za Moto kwa Maafisa wa Vyombo vya Dola na pia wanapata mafunzo ya kutosha ya haki za binadamu ili kupunguza uvunjifu wa haki za binadamu unaofanywa na polisi;
- Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani kuboresha mazingira ya utendaji kazi ya Jeshi la Polisi, ikiwa ni pamoja na vifaa, makazi na maslahi, ili kuongeza ulinzi wa haki ya usalama wa mtu;
- Asasi za kiraia, taasisi za kidini na viongozi wa kidini na kimila kutumia mamlaka yao kukemea, kuelezea madhara na kuongeza uelewa kuhusu kujuchukulia sheria mkononi, adhabu ya kifo, mauaji yatokanayo na imani za kishirikina, mashambulizi dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi na ajali za barabarani;
- Wizara ya Katiba na Sheria kuanzisha mchakato wa kupitia upya sheria zinazohusu uhuru wa kujieleza, hasa Sheria ya Huduma za Habari na Sheria ya Makosa ya Mtandaoni na kupeleka muswada bungeni ambao utapeleka vifungu vyenye utata na vinavyokiuka haki za msingi virekebishwe au kuondolewa kabisa;

- Maafisa wa Serikali na polisi kuacha kuminya haki za kiraia na kisiasa kinyume na sheria, ikiwemo kutokamata au kuweka kizuizini watu kinyume na sheria;
- Wizara ya Mambo ya Ndani, Jeshi la Polisi na Mahakama kuhakikisha kwamba maafisa wa vyombo vya dola ambao wanavunja haki za binadamu na kwenda kinyume na sheria wanawajibishwa;
- Serikali kuridhia na kutungia sheria Mkataba dhidi ya Mateso na Adhabu au Vitendo vingine vya Kikatili, visivyo vya Kibinadamu, vya Kinyama na vyenye Kudhalilisha wa Mwaka 1984 (Mkataba dhidi ya Uteswaji);
- Maafisa polisi kutumia mamlaka yao chini ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi kuhusu mikutano ya hadhara vizuri, pamoja na kutoa sababu za msingi za kuzuia mikutano hiyo kwa maandishi;
- Kama hatua ya kuboresha taasisi za kidemokrasia nchini Tanzania, Serikali isaini na kuridhia Mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora;
- Asasi za kiraia na viongozi wa Serikali kufanya kazi kwa karibu na kutoonana kama maadui ili kuboresha na kulinda haki za binadamu Tanzania;
- Serikali na Jeshi la Polisi kuweka mazingira mazuri ya asasi za kiraia kufanya kazi na kutoingilia uhuru wao wa kukusanyika kwa amani;
- Asasi za kiraia kufanya utetezi ili kuwepo na chombo huru cha kusimamia utendaji kazi wa vyombo vya dola, hasa polisi (policing the police);
- Tume ya Taifa ya Uchaguzi kufanyia kazi changamoto na dosari ambazo zinaathiri ufurahiaji madhubuti wa haki ya kushiriki kwenye utawala, hasa kwa makundi maalumu kama watu wenye ulemavu;
- Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na asasi za kiraia kuendelea kutoa elimu ya uraia na mpiga kura kabla ya Uchaguzi wa Madiwani mwaka 2019 na Uchaguzi Mkuu mwaka 2020, ikizingatiwa bado hali ya elimu hizo ipo chini;
- Maafisa wa vyombo vya dola kutotumia nguvu kupita kiasi wakati wa kampeni na chaguzi mbalimbali na badala yake kujikita zaidi katika kuhakisha usalama wakati wa chaguzi hizo; na
- Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na mhimili wa Mahakama kuhakikisha kwamba mpango wa miaka 5 wa uendelezaji wa miundombinu ya mahakama (2015/2016-2019/2020) unatekelezwa kama ulivyopangwa, ili kuboresha ufikikiaji na upatikanaji wa haki kwa Watanzania.

## Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni

- Bado mabadiliko ya kisheria yanahitajika ili kulinda zaidi haki za wanawake zinazohusiana na kumiliki mali, hasa kwa upande wa sheria za kimila ambazo zinaminya haki hizo. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inatakiwa iongoze mchakato huu kwa kushirikiana na Tume ya Mabadiliko ya Sheria;

- Serikali kufanya jitihada za makusudi kabisa katika kuwezesha wanawake kiuchumi na kuweka miundombinu itakayowezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika masuala ya kiuchumi kueleka Tanzaia ya Viwanda;
- Taasisi za Serikali zizingatie haki za binadamu zinapofanya operesheni mbalimbali ambazo zinaweza kuathiri haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni;
- Wizara ya Elimu na Ufundi iongeze juhudi kuinua kiwango cha ubora wa elimu katika ngazi zote, ikiwemo ya chuo kikuu, ili kupata vijana wanaomaliza chuo ambao wana stadi au sifa za kuajiriwa au kujiajiri;
- Serikali kuongeza bajeti za sekta muhimu kama elimu, afya na maji na kuhakikisha fedha zinakwenda sehemu husika kwa wakati;
- LHRC inaishauri Serikali kufikiria upya uamuzi wake wa kutoruhusu wasichana wanaopata mimba kurudi shuleni kulingana na matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na mikabata ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia na pia Serikali iwekeze katika kutatua changamoto katika mfumo wa elimu ambazo zinamuathiri zaidi mtoto wa kike;
- Wizara ya Elimu na Ufundi iboreshe mazingira ya watoto wenye ulemavu na watu wengine wenye ulemavu kupata elimu, ikiwemo kutengeneza au kuboresha miundombinu na kuhakikisha wana vifaa vya kujifunzia na walimu wao wana vifaa vya kufundishia; na
- Pia, Wizara ya Elimu na Ufundi iboreshe mazingira ya walimu ya kufanyia kazi, ikiwemo kuhakikisha wana nyumba bora na wanalipwa vizuri na kuhakikisha ukaguzi wa shule unafanyika mara kwa mara.

## Haki za Makundi Maalum

- Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kupeleka bungeni muswada wa kutunga sheria maalum kuhusu ukatili wa kijinsia;
- Serikali kuzingatia usawa wa kijinsia katika teuzi na nafasi mbalimbali za uongozi na utoaji maamuzi ili kuongeza uwakilishi wa wanawake;
- Serikali kutimiza wajibu wake chini ya mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa kuhusu haki za watoto kufanya mabadilko ya sheria ili kuondoa ndoa za utotoni kwenye Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971;
- Serikali kutenga bajeti itakayowezesha kutekeleza mikakati iliyojiwekea, ikiwemo utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutokomeza Aina zote za Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto;
- Asasi za kiraia na vitengo vya ustawi wa jamii kuongeza uelewa juu ya ukatili dhidi ya watoto na kuwahamasisha wanajamii kutoa taarifa za matukio ya ukatili huo kwa mamlaka husika ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria;
- Wizara ya Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera,Uratibu,Bunge, Ajira,Kazi na Watu wenye Ulemavu kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata nafasi zaidi za kupata ajira;
- Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupeleka muswada bungeni wa kutunga sheria ya haki za wazee; na

- Serikali, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora pamoja na asasi za kiraia kuboresha hali ya haki za watu wanaoishi na UKIMWI, ikiwemo kuwaelimisha wanajamii kuhusu haki za watu hao, sheria ya UKIMWI, madhara ya ubaguzi na unyapaa na upatikanaji wa huduma za afya.